

GRADE 5 END TERM 3 MARCH 2022

KISWAHILI

ZOEZI LA 1: KUSOMA KWA UFAHAMU I.

Soma fahamu hizi kisha ujibu maswali.

Mafunzo yanayofungamana na masuala ya mazingira yanastahili kupewa kipaumbele. Hivi ni kwa sababu wanadamu wanazidi kuyachafua yale yanayotuzunguka, yaani mazingira. Mwanadamu anazidi kuchafua vianzo vya maji bila aibu. Baadhi ya vianzo hivi vya maji ni pamoja na mito, bahari, visima na mabwawa. Licha ya hayo, wanadamu wanazidi kukata miti bila kupanda mingine, kama inavyoshauriwa. Elimu ya mazingira inastahili pia kufikishwa katika viwanda vinavyofusha mawingu ya moshi ili kuwasihia wahusika kutumia kawi bora zaidi.

1. Elimu ya mazingira ipewe kipaumbele kwa sababu

2. Yale yote yanayotuzunguka huitwa

3. Andika baadhi ya vianzo vya maji katika kifungu.

4. Kulingana na ufahamu, mwanadamu anayachafuaje mazingira?

5. Inashauriwa kuwa mwanadamu akikata miti,

KUSOMA KWA UFAHAMU II.

Chatu ni nyoka mkubwa sana. Anaweza kuwa na urefu wa mita tano au zaidi. Kama nyoka wale wengine, chatu huishi msituni. Anapobanwa na njaa, yeye huwala wale wanyama wengine. Akimshika mnyama, yeye hujizungusha juu yake na kujikaza kwa nguvu kama mkanda na kumwua. Baadaye, chatu huyameza mawindo yake na kukaa kwa muda mrefu bila kula tena. Anaweza kuwa hatari kwa wanadamu pia. Hata hivyo, si kawaida kusikia kuwa chatu amemwua mtu.

6. Chatu huishi _____

7. Chatu anaweza kuwa na urefu wa _____

8. Chatu huyauaje mawindo yake? _____

9. Kulingana na ufahamu, chakula cha chatu ni

10. Kulingana na taarifa ni jambo gani lisilo la kawaida kumhusu chatu?

ZOEZI LA 2: SARUFI

walihisi zamani chakula pete kusinzia

Hapa _____ za kale, palikuwa na sungura na mbwa. Wanyama hawa

11

walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Walipendana kama chanda na _____

12

Siku moja, wawili hao _____ njaa sana. Walitafuta _____ kila mahali

13

14

bila mafanikio. Baada ya kuchoka hoi, walikaa chini ya mpera na _____

15

Tunga sentensi sahihi ukitumia vinyume vya maneno.

16. Keti

17. Njoo

18. Funga

19. Vuta.

Andika mafungu haya katika hali ya umoja.

20. Magonjwa yametibiwa.

21. Mapishi yamekamilika.

22. Manyoya yametupwa.

23. Malezi yanapendeza.

Andika udogo wa sentensi zifuatazo.

24. Mbwa anabweka

25. Mto umefurika.

26. Mtu anakohoa.

27. Mti umekatwa.

Andika katika umoja au wingi.

28. Mwavuli ulipotea jana.

29. Mikoba ilishonwa leo.

30. Mchi mpya umevunjika.

Score

30

